# VYAKULA

Msingi katika vyakula na vinywaji vyote

## Ni halali

Isipokuwa tu vile vyakula vya haramu vilivyo ainishwa na ambavyo vina madhara kwa binadamu katika afya yake, mwili wake na dini yake. Mwenyezi Mungu amewakoga wanadamu kwamba amewaumbia wao vyote vilivyomo duniani ili wafaidike navyo, isipokuwa tu vile alivyowaharamishia. Amesema kuwa: *"Yeye ndiye ambaye amekuumbieni nyinyi vyote vilivyomo duniani"*. (Albaqara, aya 29)

Mimea yote inayo oteshwa na wanadamu au wanayoivuna, ikiwa ni pamoja na miti ya porini, misitu, nyasi na uyoga kwa aina zake zote

**Ni halali na zinafaa kuliwa**

**Isipokuwa tu**

**Pombe na vilevi**

Sawa viwe vimetengenezwa kwa zabibu au shairi au chanzo chochote kingine

**Dawa za kulevya**

Vyovyote kiwavyo chanzo chake; kiwe cha mmea au kemikali

**Isipokuwa tu zile zilizoharamishwa**

**Katika Qur'ani na Suna**

**Mwenyezi Mungu ametuhalalishia sisi**

**Kula nyama za wanyama na kufaidika nazo**

## VILIVYO HARAMU

| | |
|---|---|
| Nguruwe | Huyu ni mnyama haramu katika Uislamu, ni najisi kwa viungo vyake vyote na kila kinachozalika kutokana na yeye. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: *"Mmeharamishiwa mfu na damu na nyama ya nguruwe".* (Sura Almaaida, aya 3) |
| Kila mnyama mkali mwenye meno ya chonge | Makusudio ya wanyama hawa ni wanyama wote wanaokula nyama kama vile simba na chui. |
| Kila ndege mwenye makucha makali | Hawa ni ndege wote wanaokula nyama kama kipanga na tai. |
| Wadudu | Wadudu wote walioko nchi kavu hawafai kuliwa isipokuwa nzige. |
| Nyoka na panya | Ni haramu kuwala na tumeamrishwa kuwaua. |
| Punda wa mjini | Hawa ni punda ambao wanatumika vijijini kwa ajili ya usafiri na kubebea mizigo. |

## Wanyama halali

Ni aina mbili

### Anayefugika

Na kuweza kumkamata: Hawi halali kumla ila **Kwa kumchinja kisheria.**

**CHINJO LA KISHERIA:**

Ni kuchinja au kuchoma kwa kitu cha ncha kali kulikotimiza masharti ya kisheria.

**Masharti ya chinjo la kisheria ni haya yafuatayo:**

1. Mchinjaji awe miongoni mwa watu wanaoruhusiwa kuchinja; ambao ni Muislamu au Mtu wa Kitabu (Myahudi au Mkristo) ambaye amefikia balehe na akusudie kuchinja.
2. Zana inayotumika iwe inafaa kuchinjia, inayotiririsha damu na inayokata kwa makali yake, kama vile kisu.
3. Mchinjaji ataje jina la Allah kwa kusema (Bismillah) wakati mkono wake ukichinja.
4. Kukata sehemu ambazo ni wajibu kuzikata katika kuchinja. Sehemu hizo za wajibu kuzikata ni: Koromeo (sehemu ya kupitishia chakula), koo (sehemu ya kupitishia hewa), wadijaini ambayo ni mishipa miwili mikubwa iliopo katika shingo. Ni wajibu kukata sehemu zote nne au tatu katika hizo.

### Ainaye ishi porini

Na humkimbia binadamu, na haiwezekani kumkamata ili kumchinja. Huyu anakuwa halali kwa kumuwinda kwa utaratibu wa kisheria.

**Kuwinda kumewekewa masharti kadhaa. Miongoni mwa masharti hayo ni haya:**

1. Muwindaji awe na akili timamu, awe amekusudia kuwinda, awe Muislamu au Mtu wa Kitabu. Si halali kula mnyama aliyewindwa na Mpagani au mwendawazimu.
2. Mnyama awe haiwezekani kumchinja kwa sababu ya ukali wake na kuwa kwake mbali. Ikiwa mnyama inawezekana kumchinja, kama vile kuku, mbuzi na n'gombe si halali kumuwinda.
3. Zana ya kuchinjia iwe inaua kwa makali yake kama vile mshale, risasi na mfano wake, au mnyama anayetumika katika kuwinda kama vile mbwa au tai awe amefundishwa kwa namna ambayo akipewa amri anafuata na akikatazwa anakatazika.
4. Muwindaji ataje jina la Allah na kusema (Bismillah) kabla ya kuiachia zana au kabla ya kumuamuru mbwa wa kuwindia.
5. Muwindaji akimuwahi mnyama au ndege baada ya kumuwinda na kumkuta yuko hai na hajakufa ni wajibu kwake kumchinja.

## AINA ZA NYAMA

Katika migahawa na maduka

1. Kuna nyama iliyochinjwa na Muislamu au Mtu wa Kitabu kwa utaratibu wa kisheria. Nyama hii inafaa kuliwa kwa mujibu wa makubaliano ya wanazuoni wote.
2. Kuna nyama iliyochinjwa na Muislamu au Mtu wa Kitabu kwa utaratibu usiokuwa wa kisheria, Kama kunyonga na kuzamisha kwenye maji. Nyama hii ni haramu bila ya mjadala.
3. Kuna nyama ambayo imechinjwa na mtu ambaye sio Muislamu na sio Mtu wa Kitabu, Kama wafuasi wa dini ya Budha, Wahindu na watu wasiokuwa na dini. Nyama hii ni haramu. Inaingia katika kundi hili nyama inayopatikana katika migahawa na maduka ya nchi ambazo wakazi wake wengi sio Waislamu na sio Watu wa Kitabu. Hukumu yake ni uharamu mpaka itakapothibitika vinginevyo.
4. Kuna nyama iliyochinjwa na Mtu wa Kitabu na asijulikane wakati wa kuchinja. Pia nyama inayopatikana katika maduka na migahawa yao. Msingi ni kwamba nyama hii ni miongoni wanyama wao waliochinjwa. Na kauli yenye nguvu ni kwamba inafaa kula nyama hizo pamoja na kutakiwa kujibidiisha kusema Bismillahi wakati wa kula. Pamoja na hayo, ni vizuri zaidi kutafuta nyama halali ambayo uhalali wake uko wazi.

## Vyakula vya Wayahudi

KOSHER

Kusher

Maana ya neno Kusher ambalo huandikwa na Wayahudi ni kwamba chakula hicho kimefuata kanuni za chakula ambazo hutumika katika sheria yao ya Kiyahudi.

Vyakula vyote vilivyo halali kwa Wayahudi ni halali kwetu na katika sheria yetu. Hakitolewi kitu katika vyakula hivyo, kwa kadiri tunavyojua, isipokuwa pombe tu. Wao katika hilo wana ufafanuzi.

Kwa msingi huu, inafaa kwa Muislamu kula vyakula hivyo iwapo atajua kuwa havina vilevi, japokuwa jambo jema zaidi kwake ni kutafuta vyakula vya halali na kuviulizia ili kueneza utamaduni wa kutumia vitu vya halali katika jamii.

## Siagi na jibini

Maziwa hayageuki kuwa jibini isipokuwa tu kwa kuweka hamira maalumu inayoyafanya yagande na kuwa jibini. Hamira hii hupatikana katika tumbo la mnyama anayenyonya kama n'gombe na mfano wake.

1. Jibini ambayo imetumia hamira ya mnyama aliyechinjwa na Muislamu au Mtu wa Kitabu ni halali kwa makubaliano ya wanazuoni wote.
2. Jibini ambayo imetumia hamira ya mnyama aliyekufa mwenyewe ni halali kwa kauli sahihi miongoni mwa kauli za wanazuoni.
3. Ama Jibini ambayo imetumia hamira ya nguruwe ni haramu na ni najisi kwa sababu hamira ya nguruwe ni haramu na ni najisi.

## Wanyama waishio katika nchi kavu na katika maji:

Wanazuoni wametafautiana kuhusu wanyama waishio katika nchi kavu na katika bahari au mito kwamba je, katika sheria wanaunganishwa na wanyama wa nchi kavu au wanyama wa majini? Baadhi yao wamesema kuwa wanaunganishwa na wanyama wa majini na kwa sababu hiyo inafaa kula aina zote wakiwa hai na wakiwa wamekufa, madamu hawana madhara. Wanazuoni wengine wamesema kuwa wanaunganishwa na wanyama wa nchi kavu na wanapitishiwa sheria za wanyama wa nchi kavu na, kwa hiyo, inazuiwa kula kila mwenye meno ya chonge, inapasa kumchinja mwenye kuwezekana kumchinja, na inapasa kumuwinda asiyeweza kuchinjika na si halali kula aliyekufa mwenyewe. Kauli hii ni ya tahadhari zaidi.

## Vyakula vyote vya majini

Ikiwemo mimea au samaki au wanyama na ambao hawaishi isipokuwa tu ndani ya maji na kuishi kwao nje ya maji ni nadra

**ni halali na vinafaa kuliwa**

madamu havina madhara.

Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwa: *"Mmehalalishiwa vinavyovuliwa baharini na vyakula vyake".* (Sura Almaaida, aya 96) Kilichovuliwa ni kile kilichopatikana kikiwa hai, na chakula ni kile kilicho temwa na bahari baada ya kufa kwake.

Makusudio ya bahari hapa ni maji mengi. Inaingia katika msamiati huo mito, maziwa na maeneo mengine ambayo yana maji mengi.


Msanifu
Hassan Baharuon



Mafunzo yamechukuliwa kutoka katika kitabu cha

Muongozo wa Muislamu mpya
Cha mtunzi: Fahad Bahammam

Mradi wa NEW MUSLIM GUIDE

Mtayarishaji MODERN GUIDE